

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU MWENENDO WA UVIKO-19 KWA KIPINDI CHA

TAREHE 29 OKTOBA HADI 02 DESEMBA, 2022

DODOMA: 05 Desemba, 2022

Ndugu Wananchi, Serikali imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya UVIKO-19 nchini na inaendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa ugonjwa huu. Katika kipindi cha tarehe **29 Oktoba hadi 02 Desemba, 2022**, jumla ya visa vipyta **442** vimethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO – 19. Idadi hii ni kubwa ukilinganisha na takwimu za mwezi uliopita ambapo kulikuwa na visa vipyta **272**, sawa na ongezeko la asilimia **62.5**. Aidha, kwa kipindi hiki hakuna mgonjwa aliyelazwa wala kifo kutokana na UVIKO-19.

Ndugu Wananchi, Serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo ya UVIKO-19 nchini ili kuwawezesha wananchi kupata kinga kamili na hivyo kuzuia kupata ugonjwa mkali na hata kifo pale mtu anapopata maambukizi ya virusi vinavyosababisha UVIKO-19. Hadi kufikia tarehe **02 Desemba 2022**, jumla ya watu **29,123,387** kati ya walengwa **30,740,928** ambaao ni sawa na asilimia **94.7** wamepata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO- 19.

Ndugu Wananchi, Wizara inawahimiza watu wote wenye dalili za magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa kama vile homa, mafua, kikohozi, mwili kuchoka, maumivu ya viungo, kuumwa kichwa, vidonda vya koo, kupumua kwa shida kwenda vituo vya kutolea huduma za afya mapema ili kuweza kupimwa na kupatiwa matibabu stahiki. Aidha, Wizara inaendelea kutoa tahadhari kwa wananchi wote kuchukua hatua za kujikinga na UVIKO – 19 na magonjwa mengine ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na:

- a) Kupata dozi kamili za chanjo ya UVIKO - 19
- b) Kuvalaa barakoa pindi unapokuwa na dalili za mafua au kikohozi; na uwapo kwenye mikusanyiko
- c) Kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka mara kwa mara
- d) Kuendelea kuchukua hatua za kujenga mwili imara kwa kufanya mazoezi na kula vyakula bora
- e) Kujenga tabia ya kuvalaa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya endapo utajihisi u mgonjwa
- f) Kutoa taarifa za kuvalaa watu wenye dalili za magonjwa katika jamii kuititia namba ya simu ya bure **199**

Imetolewa na:

Prof. Tumaini J. Nagu
MGANGA MKUU WA SERIKALI